



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

## News Bulletin

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 39

Juni 1 - 30, 2022

### DIRA MPYA BAJETI YA SHILINGI TRILIONI 2.9 YA WIZARA YA NISHATI 2022/2023 ILIYOPITISHWA NA BUNGE

**Shilingi Trilioni 1.44** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali kwenye mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

**Shilingi Milioni 500** zimetengwa ili kufanya kampeni kubwa ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora ya kupikia pamoja na tafiti za kubaini nishati, mfumo sahihi na vivutio vya kusambaza nishati hiyo kwa maeneo ya vijijini.

Usambazaji Umeme vijijini kuongezwa kilomita mbili kwa kila kijiji tofauti na wigo wa sasa wa kilomita moja, ili kuwezesha wengi kupata umeme.

**Shilingi Bilioni 10.00** mradi wa kupeleka na kusambaza gesi asilia katika makazi ya wananchi walio katika mkuza wa bomba kuu la gesi mikoja ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mradi huu ambao ni wa kwanza nchini utakuwa wa majaribio.

**Kuanza ujenzi wa mradi wa Kuzalisha Umeme Jua wa Shinyanga – MW 150** unaogharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 9.55.**

Mradi wa kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo vya kusambaza Bidhaa za petroli vijijini kwa njia ya mkopo nafuu. Mradi huu ni wa majaribio katika kutafuta mbinu bora zaidi za kusambaza nishati ya mafuta salama na kwa bei nafuu vijijini.


Umeme kupelekwa kwenye Vijiji 35 vilivyo katika Visiwa na Maeneo Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa. Gharama ya mradi ni **Shilingi Bilioni 54.48.**

**SOMA>> HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23 UK WA 3 HADI UK 16**



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma



## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
Mhandisi Felchesmi Mramba  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
Kheri Mahimbali

**Mhariri**  
Dorina G. Makaya

### Waandishi

Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

### Msanifu Kurasa


Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma



 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

## UTANGULIZI

- Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/22 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2022/23.
- Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2022/23.
- Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kuwa Wabunge katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha. Pia ninatoa pole kwa bunge lako tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga taifa, na Mbunge wa jimbo la Ushetu; Mhe. William Tate Ole Nasha aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamukama aliyekuwa Mbunge wa viti Maalum, Mkoa wa Rukwa. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!
- Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/2023.
- Mheshimiwa Spika**, hotuba hii ina sehemu kuu mbili. Ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/22; na sehemu ya pili ni Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/23.

## UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

### ti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2021/22

- Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/22 ilikuwa **Shilingi trilioni 2.386 ambapo Shilingi trilioni 2.359** sawa na **asilimia 98.89** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 27.22** sawa na **asilimia 1.11** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.
- Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei, 2022, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi trilioni 1.820**, sawa na **asilimia 76.29** ambapo **Shilingi trilioni 1.797** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 22.83** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
- Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka 2021/22 pamoja na mambo mengine, uliongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26; Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 kuhusu upatikanaji wa nishati.
- Mheshimiwa Spika**, taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2021/22, ikiambatana na vielelezo na takwimu mbalimbali inapatikana katika sehemu B ya Hotuba yangu, kuanzia ukurasa wa pili (2) hadi ukurasa wa thelathini na nane (38). Katika sehemu hiyo tumeripoti kazi zilizofanyika na mafanikio katika maeneo yafuatayo: -
  - Miradi ya uzalishaji, kusafirisha na usambazaji wa umeme;
  - Miradi ya usambazaji umeme vijijini;
  - Uendelezaji wa rasilimali ya jotoardhi;
  - Utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati;
  - Mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG)

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

6. Ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia;
  7. Uagizaji na upatikanaji wa bidhaa za mafuta na petroli nchini; na
  8. Udhibiti wa masuala ya nishati kupitia EWURA.
10. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeeleza awali, taarifa ya kina ya masuala yote haya, ikiwemo vielelezo na viambatishi, inaweza kusomwa kwa kirefu katika hotuba kamili ya bajeti yetu kuanzia ukurasa wa pili (2) hadi ukurasa wa thelathini na nane (38).
11. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2021/22, kulijitokeza changamoto mbalimbali ambazo tunazielezea katika sehemu ya C ya Hotuba yangu, ukurasa wa ukurasa wa thelathini na nane (38) hadi ukurasa wa arobaini (40) ambapo pia tumeelezea hatua tulizochukua kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.
- MPANGO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**
12. **Mheshimiwa Spika**, sasa naomba nijikite katika kuelezea Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023. Katika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23, Wizara itaongozwa na vipaumbele vifuatavyo:
1. Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka Gridi ya Taifa katika mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na Mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project*);
  2. Kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini;
  3. Kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake;
  5. Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve*) na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund - FPSF*);
  6. Kuiimarisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO;
  7. Kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Ghala za Dhamana ya Forodha (*Customs Bonded Warehouse*) na Kituo cha Pamoja cha Kupokelea Mafuta kutoka Melini (*Single Receiving Terminal*);
  8. Kuimarisha utendaji kazi wa taasisi zinazosimamiwa na Wizara, hasa REA, TANESCO, EWURA na PBPA pamoja na huduma zinazotolewa na taasisi hizo;
  9. Kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika sekta
  11. Kufufua shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia;
  12. Kuongeza matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia (LPG) na kwenye magari na viwandani (CNG).
  13. **Mheshimiwa Spika**, Vipaumbele vya Wizara katika mwaka 2022/23 pamoja na mambo mengine, vimejikita katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020; Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa kwa Wizara kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 kuhusu Nishati.
  14. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya nishati ni moja ya mihimili ya uchumi wa nchi na ustawi wa watu wake. Bila umeme wa uhakika na mafuta ya uhakika na ya kutosheleza, shughuli za uzalishaji mali zinazorota, na uchumi unadumaa. Kwa kutambua haya, Serikali katika mwaka ujao wa fedha imeweka vipaumbele vitakavyo hakikisha sekta

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

ya nishati inahudumia uchumi na maendeleo ya nchi ipasavyo. Miradi yote na mipango na mikakati tutakayo ielezea hapa inatupeleka kwenye safari ya uchumi imara unaonufaisha Watanzania wote.

15. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza vipaumbele hivi, napenda sasa kufafanua miradi pamoja na majukumu mengine yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2022/23 kwa kila Sekta Ndogo.

(i) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) – MW 2,115**

16. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi nyingine za kiufundi zilizopangwa kufanywa, katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaongeza umahiri na weledi kwenye usimamizi wa mradi ili kuhakikisha kwamba unamalizika ukiwa katika usalama na viwango stahili na malengo yake yanatimia. Jumla ya **Shilingi trilioni 1.44** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali kwenye mradi.

(ii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185**

17. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu, ambao utagharimu **Dola za Marekani milioni 188** hadi kukamilika kwake, umetengewa **Shilingi bilioni 35** kwa ajili ya kazi za kukamilisha.

(iii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80**

18. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa nchi tatu, utaongeza uzalishaji wa umeme nchini kwa megawati 27. Tutakamilisha mradi huu katika mwaka ujao wa fedha ambapo tumetenga shilingi bilioni 9.94 kwa ajili hiyo.

19. **Mheshimiwa Spika**, pia ipo miradi iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

(i) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

muda mrefu. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kazi mbalimbali kabla ya kuanza ujenzi wa mradi.

(ii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87**

21. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu utagharimu **Dola za Marekani milioni 287.6** hadi kukamilika kwake. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itakamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 150** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

(iii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222** unaogharimu **Dola za Marekani milioni 388.22** na umetengewa **Shilingi bilioni 8** kwa ajili

ya kukamilisha kazi mbalimbali kabla ya kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

(iv) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5**

22. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, sio tu kwamba umeme wa Gridi ya Taifa utafika Kigoma, bali pia umeme unaoingia kwenye Gridi ya Taifa utazalishwa Kigoma. Fedha **Dola za Marekani milioni 144.14** za ujenzi wa mradi zimepatikana. Taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa mradi zimefikia ukingoni. Jumla ya **Shilingi bilioni 13.97** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi za awali.

(v) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 300**

23. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu una sehemu tatu: umwagiliaji, utalii na uzalishaji wa umeme, na utagharimu **Dola za Marekani milioni 795.4**. Mwaka ujao wa fedha tumetenga **shilingi bilioni 1.45** ili kukamilisha Tathmini ya Athari za Mazingira ili kukamilisha taratibu za kupata fedha za utekelezaji wa mradi.

(vi) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300**

24. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imedhamiria kuzalisha umeme wa megawati 300 Mtwara kwa kutumia gesi asilia ili kuendeleza uchumi wa mikoa ya Kusini. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1**. Fedha za kutekeleza mradi zimepatikana kutoka Serikali ya Japan. Pia tutajenga njia ya kusafirisha umeme

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

utakaozalishwa hadi Somanga Fungu mkoani Lindi. Tumetenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuanza kazi za awali.

(vii) **Katika mwaka ujao wa fedha tutaanza ujenzi wa mradi wa Kuzalisha Umeme Jua wa Shinyanga – MW 150** unaogharimu Euro Milioni 115.30. Tumetenga Shilingi Bilioni 9.55 fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme jua MW 50; na kukamilisha taratibu za ufadhili wa awamu ya pili ya MW 100.

(viii) **Katika mwaka ujao wa fedha tumepanga pia kukarabati Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale** ili kizalishe kwa uwezo wake wa MW 21 badala ya MW 10.5 zinazozalishwa kwa sasa. Tumetenga Shilingi bilioni 10.25 kwa ajili hiyo.

25. **Mheshimiwa Spika**, kuzalisha umeme ni jambo moja lakini kuusafirisha hadi kwenye maeneo ya watumiaji ni jambo lingine. Katika mwaka 2022/23, tutatekeleza miradi ya usafirishaji umeme ambayo ipo katika hatua mbalimbali kwa sasa. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) **Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze – kV 400**

26. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ambao utagharimu Dola za Marekani milioni 51.4 na Shilingi bilioni 31.9 upo katika hatua za utekelezaji ambapo kazi zilizopangwa ni kuendelea na ujenzi wa mradi ambapo jumla ya Shilingi bilioni 180.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

(ii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

27. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Arusha hadi Namanga; na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lemugur, Arusha ambapo gharama ya mradi hadi unakamilika ni Dola za Marekani milioni 258.82. Katika mwaka 2022/23, jumla ya Shilingi bilioni 7.65 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

(iii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 ya Geita – Nyakanazi**

28. **Mheshimiwa Spika**, Gharama ya mradi huu hadi unakamilika ni Euro milioni 45 ambapo kazi zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kuendelea na kazi ya usambazaji umeme katika vijiji/mitaa inayopitiwa na mradi. Jumla ya Shilingi bilioni 6.53 zimetengwa katika mwaka 2022/23 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

(iv) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Rusumo – Nyakanazi** ambapo kazi zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi ambapo fedha za ndani Shilingi bilioni 3.30 zimetengwa kwa ajili hiyo.

(v) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma** unaogharimu Dola za Marekani milioni 35. Mradi huu ambao unapeleka umeme wa Gridi mkoani Kigoma upo tayari kwenye utekelezaji. Katika mwaka 2022/23, jumla ya Shilingi bilioni 7.14 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kazi mbalimbali za utekelezaji wake.

(vi) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 33 kutoka Nyakanazi - Kakonko- Kasulu - Kigoma**

Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itakamilisha mradi huu ambao pia utafikisha umeme wa Gridi katika mkoa wa Kigoma kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.

(vii) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga**

29. **Mheshimiwa Spika**, Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 595. Fedha hizi zimepatikana. Kwa mwaka 2022/23 zimetengwa Shilingi bilioni 34.71 kwa ajili ya kazi za awali za utekelezaji ikiwemo ujenzi wa vituo vya kupozea umeme (Risada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) fedha za ndani na nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

(viii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (Standard Gauge Railway – SGR)* ambapo TANESCO kwa kushirikiana na TRC itaendelea kuhakikisha miundombinu ya umeme msongo wa kV 220 yenye urefu kwa kilomita 415 inakamilika.

(ix) *Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (Grid Rehabilitation and Upgrading)*

30. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ambao unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini utaanza kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 8.43** zimetengwa kwa ajili hiyo.

(i) *Chalinze – Kinyerezi kV 400*

31. **Mheshimiwa Spika**, Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 42.882** kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme na **Dola za Marekani milioni 71.4** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. **Shilingi bilioni 40.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia na kuanza ujenzi.

(ii) *Chalinze - Dodoma na Chalinze - Segera kV 400*

32. **Mheshimiwa Spika**, Mradi hii kwa ujumla itagharimu **Dola za Marekani milioni 285.02** ambazo zinajumuisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme. **Shilingi milioni 225.00** zimetengwa kwa ajili ya kazi za awali na ukamilishaji wa taratibu za ufadhili wa mradi.

(iii) *Chalinze – Bagamoyo na Segera - Tanga kV 220* utakaogharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 163.21** ambapo jumla ya **Shilingi milioni 50.00** zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za awali za utekelezaji wa mradi.

(iv) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda, na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda*

**Dola za Marekani milioni 200.4** kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme, na **Dola za Marekani milioni 50** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. AFDB imeonyesha niq ya kugharamia mradi huu. Katika mwaka ujao wa fedha, taratibu za kukamilisha ufadhili zitafanyika, kazi za awali kukamilisha mradi zitafanyika.

(v) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Mkuranga* utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 150** ambapo Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 4.85** kwa ajili ya kulipa fidia na kumtafuta Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuhisha Upembuzi Yakinifu wa mradi.

(vi) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme katika Mkoa wa Simiyu* unaogharimu **Shilingi bilioni 75** ambao umetengewa **Shilingi milioni 725.00** kwa ajili ya kazi za awali ikiwemo kulipa fidia wananchi watakapitiwa na njia ya umeme.

(vii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi Kyaka na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Benaco na Upanuzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kyaka.*

34. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekeleza dhamira yetu ya kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa Kagera. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 119.4** ambapo katika mwaka 2022/23 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha Tathmini ya Mazingira na Jamii; kuandaa zabuni; kufanya usanifu wa mradi; kumpata Mkandarasi wa mradi na kuanza ujenzi wa mradi.

(viii) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma.*

35. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu pia una dhamira ya kupeleka umeme wa Gridi mkoani Kigoma na utagharimu shilingi bilioni 69.7. Katika awamu ya kwanza, Serikali imetenga shilingi bilioni 25 kwa ajili ya kupeleka umeme wa uhakika wa msongo mkubwa Urambo, kukamilisha Kituo cha kupokea umeme Urambo na kulipa fidia kwa wananchi waliopitiwa na njia ya umeme.

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

(ix) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga**

36. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu pia utapeleka umeme wa Gridi ya Taifa mkoani Katavi. Utekelezaji wake, ambao utahusisha ujenzi wa njia ya umeme na vituo vya kupooza umeme Ipole na Inyonga, umekwishaanza. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga **shilingi bilioni 124** kwa ajili ya kuukamilisha. Fedha hizi zinajumuisha malipo ya fidia kwa wananchi.

(x) **Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma**

37. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 167.7** unadhamiria kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwenye makao makuu ya nchi. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga jumla ya **Shilingi bilioni 6.57** kwa ajili ya kazi za maandalizi ya utekelezaji wa mradi.

(xi) **Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project)**

38. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imetafuta muarubaini wa kadhia ya kukatika katika kwa umeme ambako kwa sehemu kubwa kunatokana na uchakavu na kutotosheleza kwa miundo mbinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Tumekuja na Mradi Kabambe wa kuimarisha Gridi ya Taifa. Mradi huu unahusu maeneo ya utekelezaji: -

- (i) Kununua na kufunga mashineumba (*transformers*) 6,000;
- (ii) Kununua na kusimika nguzo za njia za kusafirisha umeme 380,000;
- (iii) Kununua na kufunga nyaya zenye urefu wa kilomita 46,200;
- (iv) Kununua na kufunga mita za Luku 700,000;
- (v) Kujenga vituo vya kupooza umeme (*grid substations*) 14 za 220/33kV na 132/33kV;
- (vi) Kununua na kufunga mashineumba kubwa (*power transformers*) 27 za size ya 50MVA, 60MVA, 90MVA na 120 MVA;

(vii) Kujenga njia za kusafirisha umeme za urefu wa kilomita 948 za msongo wa kV 132 na kV 220.

Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka minne na unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani bilioni 1.9** sawa na takriban **Shilingi trilioni 4.420**. Katika mwaka ujao wa fedha jumla ya **Shilingi bilioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hizo **Kielelezo Na. 17** ni mchangano wa mradi huo.

## MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) itaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza nishati bora vijijini na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo. Aidha, Serikali itakamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara na kuanza kutekeleza mradi maalum wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote.

## WARATIBU WA MRADI WA REA

40. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa miradi ya kupeleka umeme vijijini na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za maendeleo ya miradi hiyo, kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali kupitia REA itaajiri waratibu wa miradi ya umeme vijijini kwa kila jimbo. Waratibu hao watakuwa kiungo cha mawasiliano na taarifa kati ya Wabunge, viongozi wa kisiasa, wakandarasi, REA na wadau wengine. Kwa kushirikiana na TANESCO, waratibu hawa watakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa viongozi ikiwemo Wabunge kuhusu maendeleo ya miradi.

## BEI ZA KUUNGANISHIWA UMEME

41. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha wananchi wanaoishi katika maeneo ya mijini yenye sifa zinazolingana na vijiji huku wakilipa bei ya kuunganishiwa umeme ya mijini. Serikali imesikia kilio chao na tayari tumeunda timu inayojumuisha Wizara ya Nishati, TANESCO na REA. Timu hii itazunguka katika miji yote na kuyabaini maeneo hayo kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika. Maeneo yatakayobainishwa na timu hiyo yatajumuishwa kwenye bei ya vijiji, yaani shilingi 27,000. Zoezi hili litafanyika nchi nzima na kukamilishwa ndani ya miezi sita.



# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA REA 2022/2023

*(i) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu  
Mzunguko wa Pili*

42. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kufikisha umeme katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na umeme. Jumla ya vijiji vitakavyofikiwa na mradi ni **3,917** na kupelekea vijiji vyote **12,345** vya Tanzania Bara kuwa vimefikiwa na huduma za umeme. Kwa sasa wakandarasi wameshaagizwa kufanya tathmini ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo vilivyokosekana kwenye wigo wa awali wa mradi.

43. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo malalamiko ambayo yana mashiko, kwamba umeme unaofika vijijini unawafikia wakazi wachache. Serikali imesikia kilio hicho na sasa ipo katika hatua za mwisho za kupata fedha zaidi kwa ajili ya kuongeza kilomita mbili kwa kila kijiji tofauti na wigo wa sasa wa kilomita moja, ili kuwezesha wengi kupata umeme.

44. **Mheshimiwa Spika**, Gharama za mradi ni **Shilingi Biloni 1,240** na wigo wa awali utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18. Katika Mwaka 2022/23, kiasi cha **Shilingi Biloni 164.54** kitatumika ikiwemo kugharamia nyongeza ya wigo wa mradi.

*(ii) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – (Hamlet Electrification Project – HEP)*

45. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kila kijiji sasa kuwa na mradi wa umeme, Serikali imeandaa mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini. Tanzania ina jumla ya vitongoji **64,760** na kati ya hivyo 37,610 bado havijafikiwa na umeme. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 6.5**. Katika Mwaka 2022/23, Serikali imetenga **Shilingi Biloni 140.00** kwa ajili ya utambuzi wa wigo halisi wa mradi na kuanza kazi ya utekelezaji wa mradi kwa awamu.

*(iii) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2B*

46. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia za usambazaji umeme zenye urefu wa kilomita 4,246 za msongo mdogo, ufungaji wa mashine umba 1,277 na kuunga wateja wa awali 95,334 katika vitongoji 1,686 katika mikoa ya Arusha, Geita, Kagera,

Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe. Gharama za Mradi ni **Shilingi Biloni 227**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kitakachotumika ni **Shilingi Biloni 24.08**.

*(iv) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2C*

47. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme msongo mdogo wenye urefu wa kilomita 6,562, kufunga mashineumba 1,932 na kuunganisha wateja wa awali 131,719 katika vitongoji 1,752 katika mikoa ya Iringa, Manyara, Mara, Mtwara, Rukwa na Ruvuma. Gharama ya mradi ni **Shilingi Biloni 100**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kilichotengwa ni **Shilingi Biloni 31.10**.

*(v) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara (220/33kV, 1 X 20MVA) na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Umeme*

48. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ifakara ujenzi wa kilomita 299 za njia za msongo wa kati na mdogo, ufungwaji wa mashineumba 26 na kuunganisha vijiji 8 na vitongoji 7 katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Gharama ya mradi ni **Shilingi Biloni 23.62** na kwa Mwaka 2022/23, kiasi cha **Shilingi Biloni 2.00** zimetengwa katika kukamilisha mradi huo.

*(vi) Mradi wa Kusambaza Umeme Maeneo ya Vijiji-Miji Awamu ya Pili (Peri-Urban)*

49. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika ni kupeleka umeme katika maeneo 153 pembezoni mwa majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kujenga njia za kusambaza umeme zenye urefu wa kilomita 751 za msongo wa kati na mdogo, ufungaji mashineumba 143 na kuunga wateja wa awali 16,328 kwa gharama ya **Shilingi Biloni 31.33**.

*(vii) Mradi wa Kufunga Mifumo ya Umeme Jua katika Taasisi za Umma katika Wilaya Nane (Sustainable Solar Market Packages Phase II – SSMP)*

50. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Sustainable Solar Market Packages ni mradi unaoendelea kutekelezwa ambapo unahusisha ufungaji wa mifumo ya kuzalisha umeme jua katika Taasisi za Umma

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

pamoja na kaya katika Wilaya za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Tunduru na Sikonge. Kazi zilizopangwa kufanyika ni kufunga mifumo ya umeme jua katika Wilaya zilizosalia za Bukombe na Biharamulo. Kiasi kitakachotumika katika Mwaka 2022/23 ni **Shilingi Bilioni 1.50** kutoka Serikali ya Tanzania.

**(viii) Mradi wa Kupeleka Umeme kwenye Vijiji katika Visiwa na Maeneo Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa**

**51. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa miradi midogo midogo (*mini grids*) ili kuzalisha na kusambaza umeme kutokana na vyanzo vya nishati jadidifu kama vile jua, upepo, maporomoko madogo ya maji pamoja na tungamotaka katika maeneo mbalimbali yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Mradi utahusisha ufungaji wa mifumo ya umeme katika vijiji 35 vilivyopo katika visiwa 47 katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa na Delta ya Rufiji. Gharama ya mradi ni **Shilingi Bilioni 54.48**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kilichotengwa ni **Shilingi Bilioni 20.00** kutoka Serikali ya Tanzania.

**(ix) Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Nishati Bora ya Kupikia Vijijini - Support to Clean Energy for Cooking in Rural Areas**

**52. Mheshimiwa Spika**, Asilimia 89 ya kaya hapa nchini hutumia kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia. Jambo hili husababisha uharibifu wa mazingira na afya za watu.

**53. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali itatekeleza mipango, mikakati na miradi ya matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia hasa maeneo ya Vijijini. Kwa ajili hiyo, tumetenga **Shilingi Milioni 500** ili kufanya kampeni kubwa ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora ya kupikia pamoja na tafiti za kubaini nishati, mfumo sahihi na vivutio vya kusambaza nishati hiyo kwa maeneo ya vijijini.

**54. Mheshimiwa Spika**, Vilevile katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutumia **Shilingi Bilioni 10.00** kutekeleza mradi wa kupeleka na kusambaza gesi asilia katika makazi ya wananchi walio katika mkuza wa bomba kuu la gesi katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mradi huu kwa maeneo ya vijijini ambao ni wa kwanza hapa nchini utakuwa wa majaribio. Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itaendelea kutoa ruzuku kwa Shirika la Maendeleo ya Petrol

na wadau wengine ili kupanua huduma hizo katika maeneo mengi zaidi.

**(x) Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza Bidhaa za Petrol Viijini kwa Njia ya Mkopo Nafuu – Credit Line Facility**

**55. Mheshimiwa Spika**, Watanzania wengi vijijini wanalipa fedha nyingi zaidi kununua nishati ya mafuta, ambayo pia sio safi na salama. Kutibu kadhia hiyo, Serikali imebuni mradi wa uwezesaji na uendelezaji wa vituo vidogo vya bidhaa za petroli kwa maeneo ya vijijini ambayo hayana vituo vya mafuta kwa njia ya mkopo nafuu. Mradi huu ni mpya na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa wigo wa mradi, kutangaza zabuni na kuwapata waendelezaji wadogo wa vituo vya mafuta vijijini ili kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Katika Mwaka 2022/23, Serikali imepanga kutumia **Shilingi Bilioni 2.00** kutekeleza mradi huu. Mradi huu ni wa majaribio katika jitihada za kutafuta mbinu bora zaidi za kusambaza nishati ya mafuta salama na kwa bei nafuu vijijini.

**(xi) Mpango wa Kuimarisha Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Miradi ya Nishati Vijijini**

**56. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupeleka umeme vijijini, bado vitongoji 37,610 kati ya vitongoji 64,760 nchini, havijafikiwa na umeme. Baada ya kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha, imebainika kuwa jumla ya **Shilingi trilioni 6.50** zitahitajika kuwezesha kupeleka umeme katika vitongoji hivyo.

**57. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwenendo wa bajeti kila mwaka ya kupeleka umeme vijijini, itachukua zaidi ya miaka 15 kufikisha umeme katika vitongoji vilivyosalia. Kwa muktadha huo, Serikali itahakikisha rasilimali fedha inapatikana ili kufikisha umeme katika vitongoji vyote.

**58. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Maalumu utakaowezesha kuongeza fedha zinazolingia katika Mfuko wa Nishati Vijijini kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa ya nishati vijijini kwa muda mfupi. Mpango huo unahusisha

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

kupata vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuongeza michango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, itaangalia uwezekano wa kupata wakandarasi watakaowezesha upatikanaji wa fedha pamoja na utekelezaji wa miradi kwa kutumia mfumo ujulikanao kama “*Engineering, Procurement, Construction Plus Financing (EPC+F)*”.

59. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutumia **Shilingi Milioni 500.00** ili kubuni, kuanzisha, uandaa na kutekeleza mikakati na mipango ya upatikanaji wa fedha za kutosha za kutekeleza miradi ya nishati vijijini kwa muda mfupi.

## MIRADI MINGINE YA REA

60. **Mheshimiwa Spika**, miradi mingine itakayotekelezwa ni Mradi wa Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati katika Maeneo ambayo Hayajafikiwa na Gridi ya Taifa; Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, Viwanda na Kilimo; na Mradi wa Kupeleka Umeme katika Miradi ya Shule Vijijini pamoja na Mahakama za Mwanzo. Gharama za kutekeleza Miradi hii, fedha zilizotengwa katika mwaka 2022/23 na kazi zitakazotekelezwa ni kama inavyooneka katika sehemu ya D3 ya Hotuba yangu.

## NDELEZAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI

61. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2022/23, Serikali itaharakisha maandalizi ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia rasilimali ya jotoardhi ambapo miradi minne ya Ngozi (Mbeya), Songwe (Songwe), Kiajo-Mbaka (Songwe) na Natron (Arusha), yenye uwezo wa kuzalisha takriban Megawati 200, itafanyiwa kazi. Jumla ya shilingi bilioni 5.18 zimetengwa kwa ajili ya kazi mbalimbali za maandalizi.

62. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imetenga kiasi cha **Dola za Marekani milioni 5.04** sawa na takriban **Shilingi bilioni 11.71** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*The National Energy Efficiency Action Plan*) unaolenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya matumizi sahihi ya nishati katika sekta za uzalishaji na matumizi bora ya nishati majumbani na katika taasisi mbalimbali.

## SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

63. **Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi, imekuwa ni azma ya nchi yetu kuingia kwenye uchumi wa gesi ambao utakuza mapato ya serikali na kuwanufaisha wananchi. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itachukua hatua madhubuti kuharakisha azma hiyo. Hatua zitakazochukuliwa katika mwaka 2022/23 kuhusu uendelezaji wa Sekta hii ni kama ifuatavyo:

(i) **Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi Asilia**

64. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23 Serikali kupitia PURA itasimamia uchorongaji wa visima mbalimbali vya gesi na mafuta hapa nchini na kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini. Lengo la kazi hizi ni kuhakikisha sheria na mikataba husika inazingatiwa.

65. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA itashamirisha shughuli za utafiti, utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi. Kwa ajili hiyo, itaanza maandalizi ya kunadi vitalu vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini kwa kutumia mikataba maalum. Vilevile, Serikali kupitia PURA itaandaa ramani ya kidijitali yenye taarifa za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini (*Interactive Digital Petroleum Activities Map*) ili kuongeza wigo wa utekelezaji wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli nchini. **Shilingi bilioni 1.69** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

## MIRADI YA UTAfutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Katika Vitalu vya Kimkakati

66. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitenga vitalu vya mafuta na gesi vya kimkakati kwa ajili ya kuipatia TPDC ili kuijengea uwezo na uzoefu. Vitalu hivyo ni Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi-Wembere, Songosongo Magharibi. Ziwa Tanganyika na 4/1B na 4/1C. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Serikali imetenga kiasi kwa shilingi bilioni 102.167 kwa ajili ya kazi mbalimbali za maandalizi ya uchimbaji wa gesi na mafuta kwenye vitalu hivyo. Serikali, kupitia TPDC, pia itaharakisha mchakato wa kuwapata wabia kutoka sekta binafsi ili kushirikiana na TPDC kuendeleza vitalu hivyo.

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

67. **Mheshimiwa Spika**, pia vipo vitalu vinavyoendeshwa na sekta binafsi ambavyo vinazalisha gesi au vimeonyesha dalili kubwa ya kuwa na gesi. Vitalu hivyo ni Ruvu, Ruvuma, Songosongo, Mnazi Bay, Kilosa-Kilombero na Vitalu Namba 1, 2 na 4. Katika mwaka 2022/23, Serikali kupitia PURA na TPDC itasimamia kuhakikisha kwamba waendeshaji wa vitalu hivi wanaviendeleza kwa mujibu wa ratiba za kwenye mikataba ili kuongeza uzalishaji wa gesi nchini.

**(i) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG)**

68. **Mheshimiwa Spika**, Imekuwa ni ndoto ya nchi yetu kwa miaka zaidi ya kumi sasa kuchakata gesi nyingi iliyogunduliwa kwenye Bahari Kuu, kwa ajili ya mauzo nje ya nchi na matumizi ya ndani. Mazungumzo kati ya Serikali na Makampuni ya Mafuta na Gesi (IOCs) yamekuwa yakikwama mara kwa mara.

69. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako tukufu kwamba hatua ya kwanza na muhimu ya mazungumzo kati ya Serikali na Makampuni ya Gesi na Mafuta kuhusu Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi (LNG) Lindi, imefanikiwa. Baada ya tarehe 9 Juni 2022, tutakuwa tayari kusaini Mkataba Hodhi (HGA) kati ya Serikali na Makampuni haya. Baada ya hapo, kwa mwaka 2022/23, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na; kukamilisha mazungumzo ya mwisho ya hatua za utekezaji wa mradi na hatimaye kushirikiana na makampuni kwenye usanifu wa awali wa kihandisi wa mradi (Pre-FEED), kabla ya hatua ya maamuzi ya mwisho ya uwekezaji.

**(ii) Mpango wa kufanya Eneo la Mradi wa LNG kuwa Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone)**

70. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukubwa pamoja na manufaa yatakayopakana katika mradi wa LNG, ikiwemo kuchochea ukuaji wa uchumi katika eneo utakapotekelezwa na kitaifa, Serikali ina mpango wa kuanzisha Ukanda Maalum wa Kiuchumi (*Special Economic Zone*) katika eneo la mradi ambapo maeneo yatatengwa na kuendelezwa kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara. Hatua hii, pamoja na kuimarisha shughuli za kiuchumi wakati wa utekezaji wa mradi, pia itawezesha manufaa ya mradi kuendelea kupatikana hata baada ya ukomo wake. Katika mwaka 2022/23, Wizara ya

Nishati kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini ya kufikia azma hiyo.

**RADI YA UJENZI WA MIUNDOBINU YA USAFIRISHAJI NA AMBAZAJI WA GESI ASILIA**

**(i) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

71. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 3.89** kwa ajili ya shughuli za usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali ya makazi na viwanda katika Jiji la Dar es Salaam ili kushamirisha matumizi ya nishati hiyo. Kwa upande wa mkoa wa Pwani, Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 5.15** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia viwandani.

**(ii) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi**

72. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa kilomita 10.04 kutoka Mnazi Mmoja ili kuwezesha matumizi ya gesi asilia katika eneo hilo. Kazi za usanifu na ujenzi wa miundombinu hii zinatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwezi Februari, 2023. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 5.49** kwa ajili ya kazi hiyo.

**RADI WA VITUO VYA CNG KWA AJILI YA MATUMIZI YA NISHATI  
HADALA WA PETROLI NA DIESELI KATIKA MAGARI NA MATUMIZI  
MENGINEYO**

**(i) Ujenzi wa Vituo vya CNG Katika Bohari za Mafuta za Serikali Dar es Salaam na Dodoma**

73. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya kujazia gesi asilia kwenye magari katika Bohari Kuu za mafuta za Serikali za Dar es Salaam na Dodoma. Lengo ni kuwezesha magari mengi zaidi ya Serikali na watu binafsi kutumia gesi asilia inayozalishwa nchini. Kwa kuanzia, magari ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zilizo chini yake yatawekewa mfumo wa kutumia gesi asilia. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa kwa ajili ya utekezaji kazi za awali za mradi huu.

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

*(ii) Ujenzi wa Kituo Mama na Vituo Dada vya CNG Katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani*

74. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo Mama (CNG Mother Station) cha kusindika gesi asilia katika mgandamizo mkubwa kwa ajili ya kuhudumia wateja wa CNG katika magari na pia kusambaza CNG kwenye vituo dada (CNG Daughter Stations) vitakavyokuwa mbali na miundombinu ya mabomba ya usambazaji wa gesi asilia. Sambamba na hilo, TPDC itajenga vituo dada vya kupokea na kuhifadhi CNG kwa matumizi ya gesi asilia katika magari, viwandani na nishati ya kupikia. Vituo Dada vitatu vya CNG vitajengwa eneo la Kiwanda cha Madawa cha Kairuki, Kibaha; Hospitali ya Taifa Muhimbili na Soko Kuu la Samaki Feri Magogoni. Jumla ya **Shilingi bilioni 23.2** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Vilevile, Serikali inakamilisha makubaliano na makampuni ya sekta binafsi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia.

## MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI

75. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ina makubaliano ya awali (MoU) na nchi za Uganda na Kenya kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania kwenda kwenye nchi hizo. Miradi yote ipo katika hatua za awali, ikiwemo matayarisho ya kufanya upembuzi yakinifu. Kwa upande wa mradi wa bomba la kwenda Uganda, Serikali imetenga **shilingi milioni 635** na upande wa bomba la kwenda Kenya **shilingi milioni 656.10** kwa ajili ya kazi mbalimbali za awali.

## MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA

*(i) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - Tanzania (East African Crude Oil Pipeline – EACOP)*

76. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kushiriki kwenye uwekezaji wa mtaji katika kampuni; kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi 9,122 wanaopisha mradi; kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi; na kuanza

shughuli za ujenzi wa mradi. Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 5.50** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

*(ii) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia*

77. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia lenye urefu wa takribani kilomita 1,710 ambalo litatumia mkuza wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la TAZAMA. Bomba litamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zambia. Kazi zitakazofanyika ni: kufanya mapitio ya nyaraka za mradi; kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii zitokanazo na utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa na Serikali kugharamia shughuli hizo.

## MRADI WA UANZISHWAJI WA HIFADHI YA KIMKAKATI YA MAFUTA (SPR)

78. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (Strategic Petroleum Reserve - SPR) unahusisha uratibu wa uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa bidhaa za mafuta kwa kipindi mahsus. Uanzishwaji wa SPR ni muhimu ili kuwezesha usalama na uhakika wa usambazaji mafuta nchini wakati wote. Ushiriki wa Serikali katika kuwezesha kuwepo kwa SPR utawezesha nchi kuwa na akiba ya mafuta muda wote na kuwezesha shughuli za uchumi kutoathiriwa na matukio yanayovuruga mwenendo wa bei za mafuta.

79. **Mheshimiwa Spika**, kama sehemu ya maandalizi, Serikali kupitia TPDC inayo maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi mafuta (tank farms) katika maeneo ya kimkakati nchini ili kurahisisha usambazaji wa mafuta kwa nyakati zote. Maeneo hayo yapo Kigamboni (Dar es Salaam), Chongoleani (Tanga), Zuzu (Dodoma), Isaka (Shinyanga), Makambako (Njombe), Kibirizi (Kigoma) na Mpanda (Katavi).

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

80. **Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya SPR ikiwemo maghala na mabomba ya kusafirisha mafuta, Serikali imeendelea kuhusisha Sekta binafsi katika hatua hii ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa uchumi wa nchi. Kwa sasa kazi mbalimbali zinaendelea ikiwemo kupitia na kuboresha hadidu za rejea za kuwapata wabia wa kimkakati, pamoja na kukamilisha usanifu wa kina wa mradi na kupata mahitaji ya fedha kwa mradi kwa ujumla.

## IWEZESHA TPDC

81. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuiwezesha TPDC kushiriki kwenye uagizaji mafuta kwa jumla, shughuli ambayo iliacha kuifanya miaka 20 iliyopita. Kupitia Benki Kuu na Wizara ya Fedha na Wizara mama ya Nishati, TPDC itajengewa nguvu ya kimtaji na kitaalam na kupewa kipaumbele kama taasisi ya kimkakati kwa nchi.

## HIRIKI WA TPDC KATIKA BIAHARA YA MAFUTA KUPITIA TANOIL

8.2 **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC inashiriki katika biashara ya usambazaji mafuta kupitia TANOIL (ambayo ni kampuni tanzu ya TPDC). TANOIL itaendelea na uagizaji wa mafuta kwa ujazo usiopungua tani 20,000 kwa mwezi. Ushiriki wa TANOIL umeimarisha ushiriki wa Serikali na kujenga uwezo wa TPDC na TANOIL katika biashara ya mafuta. Aidha, Ili kuimarisha mtandao wa usambazaji, TPDC kupitia TANOIL itajenga na kukarabati vituo vyake ili kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.04** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

83. **Mheshimiwa Spika**, TPDC pia inakusudia kuimarisha miundombinu ya uhifadhi mafuta ili kuwa na hifadhi ya mafuta ya kwake na kupunguza gharama za kukodi matenki (*hospitality*) kutoka makampuni binafsi. Kwa kuanzia, mkakati ni kukarabati Tenki namba 8 lenye uwezo wa tani 45,000 linalomilikiwa na TPDC na lililopo ndani ya hifadhi ya TIPER pamoja na matenki mengine yaliyopo katika eneo la TPDC Kigamboni. Jumla ya **Shilingi bilioni 12.11** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Baada ya ukarabati, Tenki hilo litatumiwa na TANOIL.

84. **Mheshimiwa Spika**, katika kutanua wigo wa biashara, TANOIL imepanga kununua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa na Wilaya, pia kuingia ubia na wawekezaji ambao watawekeza katika ujenzi huo. Kwa mpango

huo TANOIL inatarajiwa kuwa na viwanja 50 katika maeneo tofauti nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

## KUIMARISHA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA NISHATI

### (iii) Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Sekta Ndogo ya Umeme

85. **Mheshimiwa Spika**, ipo miradi ya umeme inayoweza kutekelezwa na sekta binafsi kwa manufaa ya umma. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza jitihada za kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi kwenye uzalishaji wa umeme. Serikali itakamilisha taratibu za kuwapata wawekezaji binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme kupitia zabuni kwa miradi ya umeme yenye jumla ya **MW 950** kwa kutumia jua, upepo na makaa ya mawe. Hadi sasa kampuni zilizokidhi vigezo baada ya mchujo zimefanyiwa upekuzi na zipo kwenye majadiliano na Serikali kuhusu mikataba ya kuuziana umeme ambapo utekelezaji utaanza mwaka 2022/23.

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na TANESCO imeandaa miradi 53 ya umeme yenye sura ya kutekelezwa kupitia Sekta Binafsi. Hadi sasa, miradi saba (7) ya umeme jua, upepo na maporomoko ya maji yenye uwezo wa kuzalisha **MW 597** ilipata wawekezaji wenye nia ya kuiendeleza. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea na hatua za utekelezaji wa miradi hiyo. **Kiambatisho Na. 19** ni miradi ya umeme iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kupitia ushiriki wa Sekta Binafsi.

## KUANDAA NA KUTEKELEZA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA YA NISHATI

87. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23 Wizara kwa kushirikiana na Wadau, itaandaa na kutekeleza Mikakati/Mipango mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Nishati. Mikakati hiyo ni pamoja na Mkakati wa Nishati Jadidifu (*Renewable Energy Strategy and Roadmap*), Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Mpango wa Utekelezaji (*Energy Efficiency Strategy and Its Implementation Action Plan*) na Mkakati wa Tungamotaka (*Biomass Energy Strategy*). Wizara pia itafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Kuendeleza

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

Sekta Ndogo ya Umeme (*Power System Master Plan*) ili kuhakikisha unaendana na mahitaji ya sasa ya Sekta na pia kutekeleza Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan*) unaohusisha Mpango wa Usambazaji wa Umeme Vijijini pamoja na Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia Vijijini.

## KUIMARISHA UTENDAJI NA UTOAJI WA HUDUMA KWA TAASISI NA WIZARA

88. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inasimamia taasisi muhimu zinazotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi na zenye umuhimu katika ufanisi wa shughuli za taasisi na wadau wengine nchini. Utendaji, ufanisi na ueledi wa taasisi hizi ni kipaumbele muhimu cha Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Kwa upande wa TPDC, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali italiimarisha shirika hili kwa mtaji na utaalim na kulifanya kuwa Shirika la kimkakati kwa uchumi wa maendeleo ya nchi yetu. Kwa upande wa EWURA, kwa udhibiti mahiri wa sekta hii nyeti, Serikali itasisitiza kujengea weledi, utaalim na uhuru wa kupata nyenzo za kufanya kazi zake bila hofu wala upendeleo. Kwa upande wa PBPA, Serikali itahakikisha kuwa watendaji wa taasisi hii wanakuwa waadilifu na taasisi inajenga uwezo wa kujua vizuri biashara ya mafuta duniani na kutoa ushauri sahihi kwa Serikali kuhusu usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini wakati wote. Kwa upande wa PURA, Serikali itaijengea uwezo ili itimize wajibu wake wa kusimamia na kukagua utekelezaji wa mikataba ya mafuta na gesi nchini. Kwa upande REA, Serikali itaiwezesha kwa rasilimali zaidi, lakini pia kujengea uwezo wa kubuni miradi mbalimbali ya nishati vijijini na uwezo wa kuisimamia na kusimamia wazabuni ili miradi imalizike kwa wakati uliokusudiwa.

89. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa TANESCO, Serikali italiwezesha na kulipa nafasi Shirika kuendelea na mageuzi yanayoendela ya kuliimarisha Shirika na kuliwezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake. Katika mwaka ujao wa fedha, Shirika linategemea kuanza utekelezaji wa mradi wa kubadilisha mita za LUKU kwa kuweka mita janja (*smart meters*) ili kuwezesha wateja kununua umeme utakaoingia moja kwa moja kwenye mita zao na hivyo kuondoa usumbufu kwa wateja na kuongeza mapato ya TANESCO. Hatua nyingine ni kurahisisha taratibu za maombi na uunganishwaji wa umeme ili kupunguza gharama na muda wa kukamilisha taratibu hizo, ikiwemo za kugongewa mihuri kwenye fomu

za maombi ya awali na kuhakikisha mfumo wa **Nikonekt** uliozinduliwa mwezi Aprili, 2022 unatumika nchi nzima kwa lengo la kuondoa usumbufu na gharama kwa wateja kufika Ofisi za TANESCO kwa ajili ya kufanya maombi ya kuunganishiwa umeme. Hatua hii itasaidia pia kuondoa mianya ya rushwa na vishoka.

90. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inatafakari namna sahihi ya kutekeleza mpango wa kubadilisha deni la TANESCO kwa Serikali kuwa hisa za Serikali (*Debt to Equity Conversion*) ili kuweka vitabu vya mahesabu vya Shirika katika hali nzuri itakayoliwezesha Shirika kupata fedha za miradi bila kutegemea Serikali.

## USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

91. **Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa shughuli zake, Wizara ya Nishati inaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Jumuiya ya nchi wahisani na wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa nchi na mashirika hayo kama ifuatavyo: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha Duniani (IMF); Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), United Bank for Africa (UBA); na Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea). Wengine ni Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa), DFID (Uingereza), Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani).

## E. SHUKRANI

92. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Felchesmi Jossen Mramba na Naibu Katibu Mkuu Bw. Kheri Abdul Mahimbali. Ni wazi kuwa katika kipindi kifupi nilichofanya nao kazi wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku na wameonesha ufanisi katika utendaji kazi zao. Napenda pia, niwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.) KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23

ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha malengo ya Wizara.

## F. HITIMISHO

93. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyobainisha awali, katika mwaka 2022/23 Wizara ya Nishati imejipanga kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Nishati, lengo likiwa ni kuhakikisha rasilimali za mafuta na gesi asilia zilizopo nchini zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya taifa letu na watu wake na kuimarisha upatikanaji wa nishati, ikiwemo iliyosafi na rafiki wa mazingira ili kuchochea kasi ya maendeleo ya viwanda, sekta ya huduma na shughuli ndogondogo za kiuchumi za wananchi. Aidha, Wizara itaendelea kutatua kero za wananchi hususan upatikanaji wa nishati ya umeme pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma.

94. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,905,981,533,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 2,823,029,576,000** sawa na **asilimia 97.15** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,655,556,128,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 167,473,448,000** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi 82,951,957,000** sawa na **asilimia 2.85** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 68,225,821,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 14,726,136,000** kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

95. **Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz). Vile vile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

96. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.





## Waziri Mkuu Majaliwa awapongeza Nishati kwa kufanya maonyesho viwanja vya Dodoma



Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa (wa kwanza kushoto), akipokelewa katika eneo la maadhimisho ya wiki ya Nishati, iliyofanyika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma. 25 Mei, 2022.



Spika wa Bunge, Akson Tulia (wa tatu kulia), akitembelea mabanda mbalimbali wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma, 25 Mei hadi 25, 2022.

### **Na Timotheo Mathayo, Dodoma**

**W**aziri Mkuu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa ameipongeza Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kufanya maonyesho ya wiki yenye lengo la kutoa fursa kwa wabunge kueleza hoja na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wao na kupatiwa majawabu.

Waziri Mkuu Majaliwa ametoa pongezi hizo wakati alipotembelea na kukagua mabanda

ya maonyesho yaliyoandaliwa na Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge Jijini Dodoma, kuanzia Mei 23 hadi 25, 2022.

Amesema ubunifu uliofanywa na Wizara ya Nishati ni mzuri kwa kuwa unasaidia kuelewa kile kinachoendelea ndani ya Wizara hiyo.

Ameleza kuwa wakati akitembelea mabanda mbalimbali alipata fursa ya kutembelea Banda la REA ambalo lina jukumu la kusambaza umeme vijijini ili kuwawezesha wananchi kupata huduma ya umeme.

Pia a ameona shughuli

mbalimbali zinazofanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Hata hivyo Waziri Mkuu aliwataka watazania kutembelea

maonyesho yaliondaliwa na Wizara ya Nishati yakijumuisha wataalam mbalimbali ili kupata fursa ya kufahamu kile kinachofanywa na Wizara na Taasisi zake.

Vilevile alieleza kuwa maonyesho hayo



Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa (wa kwanza kulia), akiwa kwenye banda la wizara ya Nishati wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, iliyofanyika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma. 25 Mei, 2022.

## Waziri Mkuu Majaliwa awapongeza Nishati kwa kufanya maonyesho viwanja vya Dodoma

yameandaliwa mahsusi kwa ajili ya wabunge, hivyo wabunge watakuwa na nafasi ya kuchangia wakiwa na uelewa mpana kuhusu sekta ya Nishati pamoja na Taasisi zake.

Alisisitiza kuwa wabunge wanahamu ya kufahamu umeme utapatikana lini katika maeneo yao, lakini pia kufahamu zaidi kuhusu suala la usambazaji, uzalishaji na usafirishaji hadi kumfikia mlaji.

Amesema ameona mfumo mpya wa kieletroniki unaonyesha uzalishaji na usambazaji

umeme na namna ambavyo watumishi wa TANESCO wanafanya kazi kwenye vituo vyote vya uzalishaji wa umeme.

Katika maonyesho hayo waziri mkuu Majaliwa alielekeza kuwa, kuna haja ya kuimarisha Wizara ya Nishati ili iendelee kutelekeza majukumu yake na kupata matokeo chanja ikiwa ni pamoja na kuwafikia wananchi katika kutatua changamoto za Umeme.

Alitumia maonyesho hayo pia kukutana na mameneja wote wa umeme, kuanzia ngazi

ya Wilaya hadi kanda na kuagiza watumike kama mabalozi katika kuwafikia na kuwatumikia wananchi kwa kuwaeleza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta ya Nishati.

Alisema kuwa ilani ya CCM inaitaka serikali kuhakikisha uzalishaji wa umeme unaimarishwa na usambazaji wake unawafikia wananchi wote nchini.

Alisema kuwa pamoja na maonesho hayo ambayo yamefanyika, Wizara ya Nishati


lazima ihakikishe inatoa matokeo chanya katika kila sekta.

Akizungumzia sekta ya gesi, ameagiza kuwa licha ya nishati hiyo kuanza kusambazwa majumbani kwa ajili ya kupikia, taasisi husika itanue wigo zaidi wa uzambazaji wa huduma hiyo ili kupunguza ukataji wa miti kwa matumizi ya mkaa na kuni.



Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa (wa kwanza kulia), akiwa kwenye banda la wakala wa Nishati Vijijini (REA) wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, iliyoafanyika katika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma. 25 Mei, 2022.

# Tanzania, Zambia kushirikiana katika umeme, mafuta na gesi



Waziri wa Nishati wa Tanzania, January Makamba (wa tatu kutoka kushoto) akiwa kwenye kikao na Waziri wa Nishati kutoka Zambia, Mhandisi Peter Kapala (wa tatu kutoka kulia). Kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Nishati Jijini Dar es Salaam leo Jumatatu, Mei 16, 2022.

## **Na Timotheo Mathayo,** **Dar es Salaam.**

**M**awaziri wa Nishati kutoka Zambia Mhandisi Peter Kapala na Tanzania, January Makamba wamekutana kwa ajili ya kuzungumzia maendeleo ya sekta ya Nishati kati ya Nchi hizo mbili zenye historia ya kuwa na mahusiano mazuri ya kidiplomasia.

Kikao hicho kimefanyika Mei 16, 2022 katika ukumbi wa Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam ambapo

kimejumuisha wataalam kutoka Tanzania na Zambia, na kimejadili masuala mbalimbali yaliyopo kwenye sekta ya Nishati kati ya mataifa hayo.

Waziri wa Nishati wa Tanzania, January Makamba alisema Tanzania imejenga kituo cha kusafirisha umeme kwenda Mikoa ya nyanda za juu kusini pamoja na kituo cha kuunganisha umeme kupeleka Zambia.

Aidha alisema kuwa katika kikao hicho mambo mbalimbali yamejadiliwa ikiwemo Mradi wa umeme

unaotoka Zambia kwenda Sumbawanga Mkoani Rukwa nchini Tanzania pamoja na changamoto zake.

Mawaziri hao pia

wamezungumzia juu ya biashara ya uingizaji wa mafuta kwa kuwa Zambia inatumia asilimia kubwa ya nishati ya Mafuta yanayopitia katika bandari za Tanzania.

Kuhusu changamoto ya bei ya Mafuta katika nchi hizo, viongozi hao wamekubaliana kutafuta njia bora ya kulipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

Makamba alisema lengo la ziara ya Waziri wa Nishati wa Zambia ilikuwa ni kutembelea Mradi wa Bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA) lililojengwa miaka ya 1960.

Awali Bomba hilo



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kutoka kushoto) akisisitiza jambo wakati wa kikao cha kujadili masuala ya Nishati kati ya Zambia na Tanzania Mei 16, 2022, katika ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Nishati uliopo jijini Dar es Salaam.

# Tanzania, Zambia kushirikiana katika umeme, mafuta na gesi

lilikuwa likisafirisha Mafuta ghafi kutoka Tanzania kwenda Zambia ambayo kwa kipindi hiki Mafuta hayo hayaagizwi, hivyo Zambia wanatumia Mafuta ya dizeli.

Bomba la TAZAMA ni ubia kati ya nchi mbili ambapo Tanzania inamiliki asilimia 33 na


Zambia ina umiliki wa asilimia 66, hivyo kuna mkakati wa kubadili mfumo wa Bomba hili ili lisafilishe mafuta ya dizeli.

Katika kikao hicho Mawaziri hao wamezungumzia Tanzania kuiuzia gesi Zambia pale itakapoanza kuzalisha gesi kutoka

kwenye visima vilivyopo kwenye bahari kuu.

Hata hivyo walizungumzia suala la ulinzi wa Bomba la TAZAMA mara tu litakapoanza kusafirisha dizeli, na wamekubaliana kuunda kamati ya wataalam kutoka nchi hizo mbili kushughulikia suala hilo.

Kuhusu nishati ya umeme, Waziri wa Nishati wa Zambia, Mhandisi Peter Kapala alisema nchi yake ipo katika maandalizi ya kuingia katika mfumo wa biashara ya umeme katika nchi za kusini mwa Afrika ambapo Tanzania imepiga hatua kubwa.



Waziri wa Nishati wa Zambia, Mhandisi Peter Kapala (wa pili kutoka kulia), akiwa kwenye kikao cha kujadili masuala ya Nishati nchini Tanzania kilichofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Nishati- Jijini Dar es Salaam. Mei 16, 2022.



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba ( wa sita upande wa kulia ) akiwa pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa tano upande kushoto), wakiwa kwenye picha ya pamoja na wageni mbambali nje ya ukumbi wa Bunge, Juni 1, 2022



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akiwasilisha Bungeni, Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2022/2023, Juni 1, 2022



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Bw. Kheri Mahimbali ( wa nne kutoka kushoto, akisalimiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Nishati nje ya ukumbi wa bunge mara baada Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Juni 1, 2022



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa Wizara na Taasisi zake mara baada ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Juni 1, 2022



Waheshimiwa Wabunge wakimpongeza, Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Bungeni jijini Dodoma, mara baada ya Bunge kupitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Tukio Juni 2, 2022



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akijibu hoja zilizowasilishwa na baadhi ya Wabunge wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu kabla ya Bunge, kupitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Tukio Juni 2, 2022.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akijibu hoja zilizowasilishwa na baadhi ya Wabunge wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu kabla ya Bunge, kupitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Tukio Juni 2, 2022.



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (wa kwanza kulia) akiwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato, ( aliyesimama), Bungeni Jijini Dodoma wakati wakifatilia na kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na baadhi ya Wabunge wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu kabla ya Bunge, kupitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Tukio Juni 2, 2022

# Wizara ya Nishati yang'ara maadhimisho wiki ya Nishati viwanja vya Bungeni

**Na Timotheo Mathayo,  
Dodoma**

**W**abunge wame-shauriwa kuitumia wiki

ya Nishati kikamilifu ili kupata majibu ya hoja na changamoto za wananchi kuhusu sekta ya Nishati inayojumuisha Mafuta, Gesi na Umeme.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Nishati, January Makamba wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati yaliyofanyika katika Viwanja vya Bunge mjini Dodoma kuanzia Jumatatu Mei 23-25, 2022.

Makamba alisema kuwa wizara kwa



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa kwanza kushoto), akizungumza na watumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakati wa maonyesho ya wiki ya Nishati, yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge, Jijini Dodoma, Mei 23 - 25, 2022.

kushirikiana na taasisi zilizochini yake zimeandaa maonyesho hayo kwa lengo mahsusi

ili wabunge waweze kupata majibu ya hoja na changamoto mbalimbali kuhusiana na sekta ya

nishati. Vilevile aliendelea kusema kuwa maonyesho hayo pia,



Naibu Spika wa Bunge, Hassan Zungu (wa pili kulia), akiwa na Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kushoto), wakiwa kwenye banda la TPDC wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, iliyofanyika viwanja vya Bunge, Jijini Dodoma, Mei 23 - 25, 2022.



Waziri wa Mazingira, Seleman Jafo (wa kwanza kulia), akisaini kitabu cha wageni waliotembelea banda la Mkoa wa Pwani la TANESCO wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati iliyofanyika Jijini Dodoma, Mei 23 - 25, 2022.

# Wizara ya Nishati yang'ara maadhimisho wiki ya Nishati viwanja vya Bungeni

yanatoa huduma kwa wananchi kupitia kwa wabunge hao ambao ni wawakilishi wa wananchi.

Alisema kuwa mabunge watumie maonyesho hayo kuuliza na kupata ufafanuzi kutoka kwa wataalam mbambali kutoka taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati ili kuweza kupata majibu ya maswali ya wananchi wao.

Katika maonyesho hayo yameshirikisha wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya kusambaza umeme vijijini inayosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ambapo Waziri Makamba amewataka

wabunge kutumia fursa hiyo kuzungumza na wakandarasi hao ili kutatua changamoto za usambazaji wa umeme katika maeneo yao, ambayo wakandarasi wanatekeleza miradi hiyo.

Makamba alisema kuwa moja ya faida ya maonyesho hayo pia ni kuwapatia muda wa kutosha wabunge hao kuuliza maswali yao yote katika kipindi hicho cha maonyesho ya wiki ya Nishati.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa REA, Wakili Julius Kalolo alisema kuwa maonyesho hayo ni maelekezo ya Waziri wa Nishati aliyoelekeza

kuwa kila mwaka wakati wa kipindi cha Bajeti ya wizara husika lazima maonyesho hayo yafanyike ili kuwapatia fursa wabunge na wananchi kufahamu maendeleo ya Miradi inayosimamiwa na Wizara hiyo.

Wakili Kalolo amesema kuwa miradi mingi inayosimamiwa na REA ipo katika hatua nzuri ya utekelezaji isipokuwa baadhi ilichelewa kutokana na mchakato wa manunuzi, lakini kwa sasa inaendelea vizuri.

Katibu wa wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Rashid Shangazi ameipongeza Wizara ya Nishati kwa

maonyesho hayo na kusema kuwa wabunge wamepata fursa ya kuongea na wataalam moja kwa moja kuliko kusubili majibu kutoka kwa mawaziri wa Nishati.

Shangazi alisema ni vizuri Wizara nyingine ziweze kuiga mfano huo wa Wizara ya Nishati ili pia wabunge waweze kupata fursa ya kukutana na wataalam wa sekta husika.

Maonyesho haya yamehudhuriwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson ambaye ametembelea mabanda mbalimbali ili kujionea huduma zinazotolewa na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati.



Naibu Spika wa Bunge, Hassan Zungu (wa nne kulia), akiwa na Waziri wa Nishati, January Makamba (wa nne kushoto) pamoja na wataalam mbalimbali wakiwa kwenye banda la Wakala wa Nishati Vijijini wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, iliyofanyika katika Viwanja vya Bunge, Jijini Dodoma, Mei 23 - 25, 2022.



Waziri wa Nishati, January Makamba, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na Katibu Mkuu wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba wakiwa katika mabanda ya Maonyesho katika viwanja vya Bunge Jijini Dodoma ikiwa ni maadhimisho ya wiki ya Nishati, Mei 23 - 25, 2022.



**Na Zuena Msuya, Lindi**

**Na Teresia Mhagama, Dodoma**

**K**atibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amepongeza Watumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kuendelea kufanya kazi kwa weledi na bidii ili kuhakikisha kuwa miradi mbalimbali ya Nishati inaendelea kutekelezwa licha ya changamoto zinazoikumba Dunia ikiwemo Uviko-19 na Vita ya Urusi na Ukraine.

Katibu Mkuu ametoa pongezi hizo tarehe 24 Mei, 2022 wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati unaofanyika jijini Dodoma ambao unajadili na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2022/2023. Mkutano huo umehudhuriwa viongozi mbalimbali wakiwemo Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa, Mwakilishi wa Katibu

## Katibu Mkuu Wizara ya Nishati apongeza Watumishi Wizara na Taasisi kwa utekelezaji wa miradi



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akiwa katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati unaofanyika jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula. Kulia kwake ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele na Mwakilishi wa Katibu Mkuu TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu.*

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa, Mwakilishi wa Katibu

Zghambo Chinula. "Nawashukuru na kuwapongeza kwa jitihada



*Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati unaofanyika jijini Dodoma. Wa Tatu kutoka kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Wa Pili kulia ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa. Wa Kwanza kushoto ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula. Kulia kwake ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele na Mwakilishi wa Katibu Mkuu TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu.*

ambazo mnaendelea kuziweka katika kazi, nafhamu Wizara hii inashughulika na masuala mengi makubwa pamoja na maisha ya watazania, tukiwa na udhaifu wowote utaonekana mapema, lakini mnajitahidi kufanya kazi kwa weledi na bidii na kuna miradi mingi ambayo tunaendelea kufanikisha vizuri." Amesema Katibu Mkuu

Alitaja miradi inayoendelea kutekelezwa na Wizara ya Nishati ni pamoja na mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao umefikia asilimia 60, utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda ambao unaendelea vizuri kwa pande zote za Uganda na Tanzania, ambapo kwa Tanzania wananchi wameshalipwa fidia, kazi za kuandaa maeneo ya kupitisha mabomba zinaendelea na muda si mrefu mabomba yatakayopitisha mafuta hayo yataanza kuchomelewa.

Kuhusu mradi wa kusindika Gesi Asilia kuwa kimiminika (LNG) ameeleza kuwa, timu kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi nyingine za Serikali pamoja na wawekezaji wanaendelea na majadiliano ambapo makubaliano ya mwanzo ya mradi huo yanatarajiwa kufikiwa kati ya Mwezi Mei na Juni mwaka huu.

Ameongeza kuwa, Wizara imeongeza nguvu na usimamizi katika kuhakikisha kuwa gesi inayopatikana nchini inaendelea kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na kwenye magari ambapo Serikali imeshakaa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji

## Katibu Mkuu Wizara ya Nishati apongeza Watumishi Wizara na Taasisi kwa utekelezaji wa miradi



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Sekretarieti ya Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati unaofanyika jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula. Kulia kwake ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele na Mwakilishi wa Katibu Mkuu TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu.*

(EWURA) ili kuweza kuwa na vituo zaidi vya kujazia Gesi ambapo Taasisi binafsi pia zinapewa kipaumbele.

Ameleza kuwa, kwa sasa TPDC wanajenga kituo kikubwa cha kujazia Gesi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo malori makubwa yatakuwa yanachukua gesi na kusambaza kwenye vituo nvingine.

Pia amesema TPDC wanajenga vituo katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Feri, Muhimbili, Kibaha na Ubungo yote hiyo ikiwa ni jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na wigo mkubwa wa kutumia Gesi

hiyo, ameongeza kuwa, Wizara ya Nishati itaonesha mfano kwani inatarajia kuwa magari yote ya Wizara yatabadili mfumo ili yaweze kutumia Gesi.

Kuhusu suala la mafuta, amesema kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na EWURA wanafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mafuta ya kutosha na amezitaka Taasisi hizo kuendelea kufanya kazi kwa weledi, uadilifu na uaminifu.

Kuhusu usambazaji wa umeme vijijini amesema kuwa, Serikali inaendelea kuweka jitihada ili wananchi waendeleo

## Katibu Mkuu Wizara ya Nishati apongeza Watumishi Wizara na Taasisi kwa utekelezaji wa miradi



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakiimba wimbo wa mshikamano katika Mkutano Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati unaofanyika jijini Dodoma.*

kusambaziwa umeme licha ya kupanda kwa bei ya alminium na shaba kutokana na Vita ya Ukraine na Urusi kwani nchi hizo ndio wasambazaji wakubwa wa bidhaa hizo zinazotumika kwenye miundombinu ya umeme. Amesema kuwa lengo la Serikali ni vijiji vyote kusambaziwa umeme

ifikapo Desemba mwaka huu.

Katika Mkutano huo, Katibu Mkuu amewataka watumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kuweza kuacha alama chanya katika maeneo yao ya kazi na pia ametaka kila mtumishi ahakiksihe kuwa eneo la kazi

linakuwa ni eneo lenye furaha ili kuweza kutumikia nchi vizuri na pia kujisomea ili kuendana na mabadiliko ya Teknolojia.

Kwa upande wake, Mwakilishi kwa Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu amempongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati kwa kuwa na ushirikiano mzuri na Watumishi wa Wizara na pia kwa usimamizi wa karibu wa miradi mbalimbali Nishati.

Lugeiyamu pia amewaasa Watumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi kutouangusha uongozi wa Wizara ya Nishati katika jitihada zake za kutekeleza miradi mbalimbali ya Nishati.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula amepongeza Serikali kwa kupandisha mishahara ya wafanyakazi kwa asilimia 23 pia amepongeza uongozi wa Wizara ya Nishati kwa kujali maslahi ya Wafanyakazi ambayo ni chachu ya Wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa ari na tija.

Chinula pia ametoa wito kwa uongozi wa Wizara kuendelea kusimamia suala la matumizi ya gesi ikiwemo kwenye magari kwani suala hilo litaleta unafuu kwa wananchi watakaotumia mfumo huo kwani gharama za uendeshaji wake ni ndogo kulinganisha na mafuta.

Aliahidi kuwa watumishi wa Wizara ya Nishati wataendelea kutoa ushirikiano kwa Uongozi wa Wizara na kuendelea kutekeleza kwa vitengo dhana ya "Kazi lendelee" ikizingatiwa kuwa nishati ni injini maendeleo ya nchini.

# Wizara ya Nishati yajibu hoja za wananchi kwenye Maonyesho



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa kwanza kushoto), akizungumza na wadau mbalimbali wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma, 23 Mei hadi 23, 2022.*

## **Na Timotheo Mathayo, Dodoma**

**W**izara ya Nishati imetumia wiki moja ya maonyesho ya Nishati kufafanua hoja mbalimbali zinayohusu sekta ya Umeme, Mafuta, Gesi pamoja na Nishati Jadidifu.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema hayo Mei 24, 2022 katika viwanja vya Bunge Jijini Dodoma

wakati alipokuwa anazungumza na waandishi wa Habari katika viwanja hivyo ambapo maonyesho ya Wiki ya Nishati yalifanyika.

Mhandisi Mramba alisema kuwa maonyesho hayo yamefikia malengo yaliyokusudiwa kwa sababu kila Mbunge aliyefika katika viwanja hivyo vya maonyesho aliridhishwa na majibu ya maswali yake aliyopata kutoka kwa wataalam.

Alisema kuwa, lengo la



**Washiriki wa maonyesho haya ni wataalam kutoka ngazi ya Wilaya hadi Taifa pamoja na wakandarasi wote wa Miradi inayotekelezwa na wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizochini yake."**

Wizara ni kuwapatia wabunge taarifa ya Miradi ya Nishati inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbambali nchini.

Alisema kuwa maonyesho hayo yamewezesha wabunge hao kupata maelezo ya kutosha ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama vile miradi wa Julius Nyerere (JNHPP), Mradi wa Bomba la Mafuta, Mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG), miradi wa kuunganisha umeme mkubwa Tanzania na Zambia (TAZA) pamoja na Mradi wa kugeuza magari yanayotumia Mafuta na kuanza kutumia gesi.

Mhandisi Mramba alisema

# Wizara ya Nishati yajibu hoja za wananchi kwenye Maonyesho



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akizungumza na wateja waliofika katika Ofisi yake wakati wa maadhimisho ya wiki ya Nishati, yaliyofanyika katika viwanja vya Bunge, mjini Dodoma, 23 Mei hadi 24, 2022.*

washiriki wa maonyesho haya ni wataalam kutoka ngazi ya Wilaya hadi Taifa pamoja na wakandarasi wote wa Miradi inayotekelezwa na wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizochini yake.

“Lengo la kuwakusanya wataalamu hawa pamoja ilikuwa ni kutaka kuwapatia wabunge majibu ya hoja zao kikamilifu badala ya kusubiri majibu kutoka kwa mawaziri ndani ya bunge”, alisema Mhandisi Mramba.

Kuhusu mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 amesema kuwa

wananchi wajiandae kupokea Bajeti mpya ambayo inalenga kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utekelezaji wa miradi katika wizara na taasisi zake zote pamoja na ushiriki wa sekta binafsi.

Mhandisi Mramba alisema katika miaka iliyopita hali ya changamoto ya upatikanaji umeme nchini ilikuwa kubwa lakini kwa sasa inaridhisha na Wizara inaendelea kuleta Miradi ambayo haitegemei mvua, lengo ni kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa hasa inapotokea

upungufu wa mvua nchini.

Alifafanua kuwa ili kuendelea kuwa na umeme wa uhakika nchini, Wizara kupitia Shirika la Umeme nchini (TANESCO) inakamilisha Mradi wa upanuzi wa Kinyerezi 1 ifikapo mwezi Juni 2022, ambapo jumla ya Megawati 70 zitazalishwa. Pia kufikia mwishoni mwa mwaka huu Mradi wa kuzalisha megawati 115 nyingine kutokana na gesi asilia zitakuwa zimekamiliika.

Alisema kuwa kufikia mwishoni wa mwaka 2023 Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere utakamilika.

Kuhusu Sekta ya Umeme jadidifu, shirika la umeme nchini TANESCO lipo kwenye hatua mbambali za kuingia Mikataba na makampuni yatakayozalisha umeme wa jua pamoja na umeme utokanao na upepo wenye jumla ya Megawati 350, hata hivyo TANESCO itajenga mitambo yake ya kuzalisha umeme jua itakayozalisha megawati 150.

Kaimu meneja wa taasisi ya uendelezaji joto ardhi nchini, (TGDC), Mhandisi Shakiru Kajuna alisema taasisi hiyo inaendelea na mipango ya kupata umeme utokanao na joto ardhi, ambao inategemea kuzalisha megawati 200 ifikapo mwaka 2025.

# Kamati ya Makamba ya kufuatilia nguzo za miti zenye ubora yaanza kazi rasmi

**Na Mwandishi MoE**

**K**amati Maalum iliyoundwa na Waziri wa Nishati, January Makamba ya kufuatilia nguzo za Miti za Umeme zenye ubora imeanza kazi rasmi kwa kutembelea viwanda 25 katika Mikoa ya Iringa na Njombe.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga amesema Lengo la ziara hiyo ni kufanya tathmini ya viwanda hivyo na kuona kama vina uwezo wa kuzalisha nguzo zenye ubora na kutosheleza mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Kamati hiyo imefanya kazi ya kutembelea viwanda hivyo kwa siku 7 kuanzia terehe 9 hadi 15 mwezi Mei, 2022 kwa utembelea viwanda 25 vya kuzalisha nguzo za miti vilivyopo katika Mikoa ya Iringa na Njombe.

Mhandisi Luoga amefafanua kuwa katika ukaguzi huo, Kamati hiyo imebaini masuala mbalimbali yanayohitaji kufanyiwa kazi kwa haraka.

Ametaja baadhi ya masuala hayo ni pamoja na ukosefu wa vifaa vya



*Picha mbalimbali za wajumbe kamati maalum ya kufuatilia nguzo za Miti za Umeme zenye ubora*

# Kamati ya Makamba ya kufuatilia nguzo za miti zenye ubora yaanza kazi rasmi



**Kamati hiyo imewataka Wadau wa nguzo za miti kuhakikisha wanazalisha nguzo zinazokidhi viwango na ubora unaotakiwa kimataifa ili kuweza kukidhi soko la ndani na hata nje ya Nchi kwa kuwa mikoa hiyo inaongoza katika uzalishaji wa miti ya nguzo.”**

kupima ubora nguzo, upatikanaji wa soko la ndani na nje, miche ya miti inayokuwa haraka pamoja madawa yasiyo na ubora.

Awali, Waziri Makamba alisema kuwa Lengo la Serikali ni kukuza uchumi wa wananchi wake kwa kuboresha bidhaa zao kwa kuwasimamia



katika kuzalisha kwa vigezo vya ubora na viwango vinavyotakiwa ili wananchi hao waweze kunufaika na kukuza uchumi wao na pato la Taifa kwa ujumla.

Hivyo, Kamati hiyo imewataka Wadau wa nguzo za miti kuhakikisha wanazalisha nguzo zinazokidhi viwango na ubora unaotakiwa kimataifa ili kuweza kukidhi soko la ndani na hata nje ya Nchi kwa kuwa mikoa hiyo inaongoza katika uzalishaji wa miti ya nguzo.

Kamati itaendelea kufuatilia ubora wa nguzo na kutoa ushauri

sahihi kwa Wadau hao juu ya njia bora za kufuata na kuzingatia ili kupata bidhaa zilizobora zitakazo kubalika Kitaifa na kimataifa.

Aidha Mwenyekiti wa Kamati aliwataka Wadau wa nguzo waungane pamoja ilikuleta Umoja wenye nguvu na tija kwa maslahi mapana ya nchi.

Kamati hiyo imeshirikisha maafisa kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Viwango Nchini (TBS).

Wajumbe wengine ni kutoka Umoja wa Wazalishaji wa Nguzo

za Miti nchini, Umoja wa Wauza nguzo nchini, Umoja wa Wakulima wa Nguzo, Taasisi ya Panda Miti Kibiashara, Mfuko wa Maendeleo ya Mimitu pamoja Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

Baadhi ya Viwanda vilivyotembelewa ni pamoja na vinavyimilikiwa na Shedafa, Agora, TANWAT, New Forest, Sao Hill, Poles Manufacturer, Qwihaya pamoja na DN.

Kamati hiyo itaendelea na ziara yake katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Mara na Dar Es Salaama.

# Makamba awahakikishia soko la ndani Wadau wa nguzo za Umeme za Miti nchini

**Aunda Kamati maalum itakayoweza upatikanaji wa nguzo zenye ubora zaidi**



Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na Wadau wa nguzo za miti (hawapo pichani), kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa Queen Sendiga, katika mkutano wake na wadau hao uliofanyika, Mafinga mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.

## **Na Zuena Msuya,** **Iringa**

**W**aziri wa Nishati, January Makamba amewatoa hofu wadau wa nguzo za Miti za Umeme nchini kwa kuwahakikishia soko la kuuza nguzo zenye ubora kwa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini ( REA),

hapa nchini.

Aidha, amewataka Wadau hao kuzalisha nguzo hizo zenye ubora ili Serikali iweze kuwatafutia masoko ya nje kwa kuwa wana uwezo kuzalisha zaidi kukidhi mahitaji ya soko la ndani ya sasa na ziada.

Makamba alisema hayo wakati wa mkutano wake uliohusika Wazalishaji, Wasafirishaji, na Watengenezaji wa nguzo za miti za Umeme,

kutoka Mkoa wa Iringa na Njombe, uliofanyika Mafinga Mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.

Mkutano huo umelenga kuondoa sintofahamu pamoja na minong'ono inayoendelea kwa baadhi ya watu wanaopotosha kuwa Serikali haitanunua nguzo za Umeme za ndani na badala yake zitaagizwa kutoka nje ya Nchi.

Katika mazungumzo

yake na Wadau hao, Makamba alisema kuwa, Serikali itaendelea kununua nguzo za miti za Umeme kutoka kwa wazalishaji wake wa ndani ili kulinda viwanda vya ndani kwa kuzingatia ubora wa nguzo uliowekwa.

“Lengo la Serikali ni kukuza uchumi wa wananchi wake kwa kuboresha bidhaa zao kwa kuwasimamia katika kuzalisha kwa vigezo na ubora uliowekwa, ili wananchi hao waweze kunufaika na kukuza uchumi wao na pato la Taifa kwa ujumla”, Alisema Makamba.

Pamoja na Mambo mengine, aliwataka Wadau hao kuhakikisha wanazalisha nguzo zinazokidhi viwango na ubora unaotakiwa kimataifa ili kuweza kukidhi soko la ndani na hata nje ya Nchi kwa kuwa mikoa hiyo inaongoza kwa kuwa na uzalishaji wa nguzo.

Alisema kuwa, Serikali itakikisha kuwa biashara ya nguzo za miti za Umeme, inakuwa zaidi Kitaifa na kimataifa kama Nchi zingine zinavyofanya ikiwemo Afrika Kusini ambao



## Makamba awahakikishia soko la ndani Wadau wa nguzo za Umeme za Miti nchini



*Baadhi ya Wadau wa Nguzo wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba( hayupo pichani), wakati wa Mkutano wa Waziri huyo na wadau hao kuhusu uzalishaji wa nguzo bora uliofanyika, Mafinga mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.*

wanauza nguzo kama hizo katika nchi nyingine.

Kwa Mantiki hiyo, ameelekeza kuundwa kwa Kamati ya watu 12 kutoka katika kila kundi la Wadau wa nguzo za miti za Umeme, katika Mikoa ya Njombe na Iringa, Wizara na Taasisi zake pamoja na Shirika la Viwango nchini (TBS) ili kuongeza ufanisi katika kuzalisha nguzo zenye ubora unaolidhi viwango.

Kamati hiyo pia itotoa ushauri sahihi kwa Wadau hao juu ya njia bora za kufuata na



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), Maharagwe Change, akizungumza na Wadau wa nguzo( hawapo pichani) wakati wa mkutano wa Wadau hao kuhusu uzalishaji wa nguzo bora uliofanyika, Mafinga mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.*

kuzingatia ili kupata bidhaa zilizobora zitakazo kubalika Kitaifa na kimataifa.

Waziri Makamba amewataka Wadau hao kuunda chama Cha wazalishaji wa nguzo ili kiweze kudhibiti ubora unaotakiwa na hata kutoa adhabu kali kwa atakayebainika kuzalisha chini ya Kiwango pamoja na kuandaa sheria zitakazoongoza chama hicho.

Aidha ameutaka umoja huo kwenda kujifunza zaidi, namna ya kudhibiti ubora wa nguzo kwa nchi zilizofanikiwa ikiwemo Afrika Kusini ili kuleta ushindani zaidi.

“Ni vyema mkawa na Cha ma chenu kinachotambulika kisheria, Cha hiki ni chombo muhimu katika kuwasimamia na kuwaongoza, vilevile kitakuwa kinatumika kudhibiti ubora wa nguzo zinazozalishwa kwani atakayekuwa akienda tofauti mtamshungulikia na hata kumpatia adhabu pale atakapokuwa akienda kinyume na kuharibu soko”, Alisisitiza Makamba.

## Makamba awahakikishia soko la ndani Wadau wa nguzo za Umeme za Miti nchini



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Said, akizungumza na Wadau wa nguzo (hawapo pichani) wakati wa mkutano wa Wadau hao kuhusu uzalishaji wa nguzo bora uliofanyika, Mafinga mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharagwe Change, aliwataka Wadau hao kuwa waaminifu pale nguzo zao zinapotakiwa kupelekwa katika maeneo ya miradi kwa kuweka nguzo halisi zilizokaguliwa na siyo kufanya udanganyifu wa kuweka zisizokuwa na ubora.

Amesema kumekuwa na changamoto ya nguzo kuharibika baada ya muda mfupi kutumika kutokana na kuwa chini ya kiwango

na ubora unaotakiwa,

huku nguzo hizo zikiwa tayari zimekaguliwa na kuonekana zina ubora unaotakiwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Said, amewahakikishia Wadau hao kuwa soko la nguzo lipo la kutosha kwani bado miradi mingi ya usambazaji wa Umeme vijijini inaendelea na nguzo nyingi zinahitajika.

Akitoa mfano Mkoa wa Iringa kuwa kuna Mradi wa Ujazilizi ambao unatarajia kuanza hivi karibuni katika Mkoa huo na miko mingine.

Katika hatua nyingine,

Mwenyekiti wa Mkutano huo ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alimuhakikishia Waziri wa Nishati kuwa atashirikia na Wadau hao kutekeleza yake yanayotakiwa ili kupata bidhaa Bora na hatimae Mkoa hiyo iwe kinara katika kuzalisha nguzo na bidhaa za miti zenye ubora unaotakiwa.

Amewataka Wadau hao kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika na kuwa wasikivu kwa kile watakachokuwa wakielezwa kwa lengo la kupata bidhaa Bora kwa manufaa yao na taifa kwa jumla.



Mbunge wa Mfinga ambaye ndiye mwenyeji, Cosato Chumi, akizungumza wakati wa mkutano wa Wadau wa Nguzo, kuhusu uzalishaji wa nguzo bora uliofanyika, Mafinga mkoani Iringa, Aprili 30, 2022.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)